Kuota unafanya tendo la ndoa au kuota unafanya mapenzi na mtu usiyemjua maana yake ni nini?

---

Awali ya yote tunapaswa kufahamu kuwa Ndoto yoyote ya zinaa, haitokani na Mungu..Ni aidha inatokana na mtu mwenyewe au shetani. Leo tutaangazia makundi mawili ya watu wanaoota ndoto za namna hii:

**Kundi la kwanza ni: Kwa mtu ambaye hajaokoka:**

Biblia inasema..

> *Mhubiri 5:3 "Kwa maana ndoto huja kwa sababu ya shughuli nyingi;..."*

Hii ikiwa na maana kuwa, yale mambo au vile vitu tulivyokuwa tunavifanya au kuvifikiria mchana kutwa mara nyingi huwa ndio hivyo hivyo tunaviota tukiwa tumelala..

Hata kama hatutaviota vilevile kama vilivyo lakini tutaota mambo

yanayoendana na matukio tuliyokuwa tunayafanya katika mazingira yanayotuzunguka..Kwamfano kama wewe wiki nzima ulikuwa unashinda mashambani tu kulima na kupalilia shamba lako..Uwezekano wa wewe kuota upo shambani unafanya shughuli kama hizo ni mkubwa sana..Kama wewe ulikuwa shuleni mwaka mzima bwenini uwezekano wa kuendelea kuota ndoto upo shuleni ni mkubwa..

Vivyo hivyo kama wewe ni mlevi unayeshinda bar kila siku usiku uwezekano wa kuota ndoto za upo bar unakunywa pombe na marafiki zako ni mkubwa..Haiwezekani mtu ambaye hajawahi kuenda bar au kunywa pombe Maisha yake yote akaota anakunywa pombe bar na akalewa. Vivyo hivyo hata katika zinaa, kama Maisha yako yote, na wakati wako wote unawaza uzinzi kichwani, unatazama picha chafu mitandaoni, na video za pornography, unafanya mustarbation, unaangalia muvi za mapenzi, unasiliza nyimbo za kidunia za kizinzi, maneno unayozungumza kila mara ni ya usherati tu, jinsi ya kumpata binti yule au kaka yule..Nataka nikuambie kila siku usiku kuota unafanya tendo la ndoa au unafanya mapenzi na mtu usiyemjua au unayemjua itakuwa ni jambo la kawaida kwako.

Kwasababu Maisha yako yote yapo katika uzinzi..Shughuli kubwa iliyo katika ubongo wako ni zinaa..

Vilevile yapo mapepo ya namna hii mahususi kutoka kuzimu yanawavaa watu ambao hawajaokoka ili kuchochea hii hali ndani yao. Ndio hapo utamwona

mtu ndoto kama hizi zinakuwa ni sehemu ya Maisha yake, anajikuta mara kwa mara anafanya mapenzi na mtu asiyemjua, leo,Kesho, anapumzika wiki moja hali ile ile inajirudia tena na tena, ukiona hivyo ujue lipo pepo limeshakuvaa.

Unahitaji kugeuzwa Maisha yako.

**Kundi la Pili: Kwa mtu aliyeokoka.**

Lakini kama wewe upo ndani ya Kristo.

Mambo mawili yanaweza yakawa yanahusika.

La Kwanza. Ni ishara ya kuwa kuna mahali unapoa,.Umepunguza kiwango chako cha nguvu za rohoni, kuna mahali unapadokoa au baadhi ya mambo kidunia yanakuchukua..Hivyo hapo unapaswa uongeze bidii yako kwa Mungu, ongoza kiwango chako cha maombi, tumia muda mrefu kusoma biblia kuliko kufuatilia mambo yasiyokuwa na maana. Simama imara katika Imani yako. Kabla hujalala jijengee utaratibu kwa kuomba. Na hiyo hali haitajirudia tena.

Lakini kama wewe umeokoka na bado unauhakika umesimama imara katika Imani, na ndoto kama hiyo imekujia bila kutazamia, na ishara kuwa ulikuwa hufurahii ni kwamba hata katika hiyo ndoto ulikuwa unaonyesha upinzani,kukataa hicho kitendo, au kujiuliza inakuaje kuaje nipo katika hali

hii na mimi nimeokoka.. basi hali kama hiyo ikikujia Ikimee mara moja kwa jina la YESU, kisha mwambie shetani huwezi kunijaribu kwa kishawishi chochote..Na ndoto kama hizo hutaziota tena..

Jambo ambalo watu wengi hawafahamu ni kuwa zinaa, kuiondoa ndani ya mtu inahitaji muujiza, na anayeweza kuikata kiu hiyo ni YESU KRISTO peke yake, haijalishi wewe ni mkristo au wewe ni muislamu au hauna dini ..Ni Yesu pekee ndio anayeweza kukubadilisha na kukufanya uishi Maisha yaliyo mbali na zinaa.

Dhambi hii, inawashinda wengi, na ndio dhambi inayoongoza kuwapeleka watu kuzimu. Isitoshe biblia inasema, Kama vile ilivyokuwa katika siku za Sodoma na Gomora ndivyo itakavyokuwa siku za kuja kwake mwana wa Adamu. Kumbuka siku za Sodoma na Gomora, kulikuwa na uzinzi wa kiwango vya hali ya juu kama vilivyopo sasa, kulikuwa kuna mashoga na wasagaji waliokuwa wanajidhirisha waziwazi kama ilivyo sasa.. Na hiyo ndio ikiwa sababu ya miji ile kuteketezwa..Lakini cha kuogopesha Zaidi ni kwamba, kati ya maelfu kama sio mamilioni ya watu waliokuwa katika miji ile, ni watu watatu tu ndio walionusurika..wengine wote waliteketea kwa moto..

> *Luka 17:28 “Na kadhalika, kama ilivyokuwa katika siku za Lutu, walikuwa wakila na kunywa, walikuwa wakinunua na kuuza, wakipanda na kujenga;*
>
> *29 lakini siku ile Lutu aliyotoka Sodoma kulinyesha moto na kibiriti kutoka mbinguni vikawaangamiza wote.*
>
> *30 Hivyo ndivyo itakavyokuwa siku ile atakayofunuliwa Mwana wa Adamu”*

Soma tena kwa makini mstari huu:

> *Yuda1:7 “Kama vile Sodoma na Gomora na miji iliyokuwa kando-kando, waliofuata uasherati kwa jinsi moja na hawa, wakaenda kufuata mambo ya mwili yasiyo ya asili, imewekwa kuwa dalili, wakiadhibiwa katika moto wa milele.*
>
> *8 Kadhalika na hawa, katika kuota kwao, huutia mwili uchafu, hukataa kutawaliwa, na kuyatukana matukufu”.*

Unaona? Vivyo hivyo na jambo kubwa Zaidi litakalofanya ulimwengu huu uteketezwe siku ambazo si nyingi, ni dhambi ya zinaa, vilevile watakaonusurika watakuwa ni wachache sana. Mungu huwa hana wengi wape,.Leo hii unaweza kusema mbona kila mtu yupo hivi au yupo vile..Lakini nataka nikuambie  hata kama dunia nzima imeamua kuasi Mungu akimuona mtu mmoja tu, inatosha yeye kuangamiza..

Hivyo ikiwa wewe ni mwenye dhambi, haijalishi dini yako, au dhehebu lako.Yesu anawaokoa watu wote, na bado anaendelea kuokoa ikiwa mtu atakuwa tayari kutaka kuokolewa naye, kwasababu neema yake kaiachia kwa watu wote. Ikiwa leo hii unataka kusema Maisha ya uzinzi basi, nataka YESU anasaidie niishinde dhambi hii na nyingine zote…Ukiwa unamaanisha kweli kufanya hivyo..Basi leo hii hapo ulipo anaweza kukuokoa na kukugeuza na kukufanya kuwa mtoto wake.

Ikiwa upo tayari kubadilishwa leo Maisha yako na Yesu..Basi fahamu kuwa yeye yupo hapo pembeni yako kukusaidia, unachopaswa kufanya ni kufungua tu moyo wako..Uhitaji unione mimi, au usikie sauti yangu..Suala la wokovu ni Zaidi ya upeo wa fikra za kibinadamu. Leo hii YESU atayageuza Maisha yako, na atafanya muujiza mkubwa ndani yako kwa namna ambayo hujawahi kuidhania.

Hata na yale mengine mbali na uzinzi, labda ulevi, matusi, wizi yote atayaua ndani yako ikiwa tu utakuwa tayari kumpokea Leo. Yesu yupo hai, yupo

tayari kwa mtu yeyote kumsaidia wakati wowote bure.. hivyo bila kukawia kawia hapo ulipo chukua muda jitenge eneo la utulivu. Kama upo ndani tafuta chumba ujitenge peke yako, kisha piga magoti..Ukiwa hapo chini umepiga magoti sema sala hii kwa sauti..

EE MUNGU BABA, NAJA MBELE ZAKO, NIKIWA NINAJITAMBUA KUWA MIMI NI MKOSAJI NA NIMEKUTENDA DHAMBI NYINGI, NA KWAMBA NIMESTAHILI HUKUMU. LAKINI WEWE MUNGU WANGU ULISEMA KATIKA NENO LAKO KUWA WEWE NI MUNGU WA REHEMA UNAYEWAREHEMU MAELFU ELFU YA WATU WANAOKUPENDA WEWE. NA LEO HII NINAKUJA MBELE ZAKO NAHITAJI MSAMAHA WAKO NA MSAADA WAKO MUNGU WANGU WA KUSHINDA DHAMBI, NINATUBU DHAMBI ZANGU ZOTE KWA KUMAANISHA, NA KWA MOYO WANGU WOTE, NINAKIRI KUWA YESU KRISTO NI BWANA, NA YEYE NDIYE MWOKOZI WA HUU ULIMWENGUNI. HIVYO NAOMBA DAMU YA MWANAO TAKATIFU INISAFISHE UOVU WANGU WOTE SASA NIFANYIKE KUWA KIUMBE KIPYA KUANZIA LEO NA HATA MILELE.

ASANTE BWANA YESU KWA KUNIPOKEA NA KWA KUNISAMEHE.

*AMEN.*

Sasa ikiwa umefuatisha sala hiyo kwa Imani Mungu amekusikia ..Hatua iliyobakia kwako ni kuithitisha toba yako kwa matendo, hapo ulipo ikiwa

ulikuwa na picha chafu katika siku yako, anza kwa kuzifuta, ikiwa ulikuwa unayafanya mambo yote ambayo hayampendezi Mungu unayaacha na kujitenga nayo, Sasa Mungu akishaona umegeuka kwa vitendo basi toba yako anaipokea na atakuja ndani yako wakati huo huo na kufanya makao ya milele kwako. Kuanzia leo hii utaanza kuona badiliko kubwa ndani yako. Jambo lingine unalohitaji kufanya ni kutafuta kanisa la kiroho ambalo utajumuika na wakristo wengine katika kumwambudu Mungu, na katika kujifunza biblia ili uukulie wokovu.

Hata kama wewe ulikuwa ni muislamu, tafuta kanisa lililokaribu na wewe la kiroho, waeleze uamuzi wako uliouchukua, kisha wao watakuelekeza hatua inayofuata au kama utahitaji msaada wa kanisa kwa eneo lako basi wasiliana nasi kwa namba hizi **0789001312**.. Ili upate ubatizo sahihi wa kuzamishwa katika maji mengi na kwa jina la YESU KRISTO kwa ajili ya ondoleo la dhambi zako.

Yazingatie hayo. Na Bwana atakuwa pamoja na wewe katika kila hatua ya Maisha yako. Na ndoto zote hizo za Kuota unafanya tendo la ndoa au kuota unafanya mapenzi na mtu usiyemjua, zitaisha.

jiunge na channel yetu Kwa kubofya hapa >> **WHATSAPP**

**Mafundisho mengine:**

Bwana akubariki.

**Kwa mgawanyo bora wa masomo download App hapa>> App wingu la mashahidi**

Pia zidi kutembelea website yetu hii, kwa mafundisho mengine

**Mada Nyinginezo:**

> *Nitajuaje kama ndoto ni ya Mungu au ya Shetani?*

> *KUOTA UPO UCHI.*

> *KUOTA UNAKULA CHAKULA.*

KUOTA UNAFANYA TENDO LA NDOA.

*Kuota unafanya Mtihani.*

*Kuota unakimbizwa.*

*MKUU WA ANGA.*

*UNAWAFAHAMU MANABII WA UONGO?*

*SIKU YA UNYAKUO ITAKUKUTAJE?*

*KIFO CHA REINHARD BONKEY KINAACHA UJUMBE GANI KWETU?*

## Rudi Nyumbani:

Share on:
WhatsApp